Moto umezingirwa na yenyekutamanisha, na Pepo imezingirwa na yenyekuchukiza

Imepokelewa Kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake- Yakwamba Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Moto umezingirwa na yenyekutamanisha, na Pepo imezingirwa na yenyekuchukiza".

[Sahihi] [Imepokelewa na Al-Bukhaariy]

Amebainisha Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa Moto umezungukwa na kuzingirwa na mambo ambayo nafsi inayatamani, kama kufanya maharamisho au uzembe katika mambo ya wajibu; Atakayeendekeza matamanio ya nafsi yake katika hilo atastahiki moto, nakuwa Pepo imezungukwa na kuzingirwa na mambo ambayo yanachukiwa na nafsi; kama kudumu katika maamrisho na kuacha maharamisho na kuvumilia juu ya hilo, atakapovumilia na akapigana vita na nafsi yake juu ya hilo atastahiki kuingia Peponi.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/3702